
MTAALA WA UMILISI

KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI

GREDI 5 - MWAKA 2021

SILVER

SHUGHULI ZA KISWAHILI



Jina _____

Jina la shule _____

VIWANGO VYA KUTATHMINI			
Kuzidisha matarajio	Kufika matarajio	Kukaribia matarajio	Mbali na matarajio
40-45	29-39	15 - 28	0 - 14

SEHEMU YA KWANZA **(Alama 5)**

KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu amuamkue mwanafunzi,amkaribishe,ajitambulishe kwa mwanafunzi kisha waanze mazungumzo:mapishi

1. Taja kifaa kimoja kinachotumika kwa upishi jikoni_____
2. Mtu anayepika jikoni huitwa?_____
3. Taja vyakula viwili vinavyopikwa jikoni

   _____ _____
4. Jiko la makaa huitwa_____
5. Taja umuhimu mmoja wa chakula mwilini_____

SEHEMU YA C **(Alama 10)**

Mwalimu amsomee mwanafunzi kisha ajibu maswali.

Ni muhimu kuhakikisha mazingira yanawekwa safi. Hebu kwanza tuone nyumbani. Hapa ndipo mazingira yanapoanza. Kitanda kitandikwe vizuri, nyumba ifagiliwe kwa usawa, madirisha yafunguliwe ili kuwe na hewa safi na jua lipenye hadi ndani ya nyumba ili wadudu wabaya wahame.

Nyasi ndefu ni lazima zikatwe ili kupunguza mbu. Takataka lazima zizikwe wakati zinapokusanya ili wadudu kama nzi wasipate nafasi ya kuletea uchafu na magonjwa kama ya kuendesha mikebe iliyo wazi kandokando ya nyumba na ambayo inaweza kujaa maji na kuwafanya mbu wazaane lazima itupwe mbali. Kwenye miji, vyoo ni lazima viwekwe safi ili matatizo yasiweze kupatikana hasa ya maradhi. Ni jambo lisilofaa kutokuwa na choo nyumbani. Ni muhimu watu wawe na vyoo. Hii itakuwa ni njia moja ya kuokoa mazingira yasiharibike. Miti hurembesha nchi, hutupatia mbao za kujenga nyumba na pia huhifadhi wanyamapori.